# KUMILIKI MALANGO YA ADUI

Habari za asubuhi kila mtu na ninafurahi kurudi asubuhi hii hapa Maskanini kuwaombea watu Walio wagonjwa leo. Ni kawaida yangu kujaribu kuingia mara kwa mara kwa mara na—na kuwaombea watu wanaokuja kutoka mahali mbali mbali kwa ajili ya maombi. Na sasa tutaondoka hivi karibuni kwa mikutano ya California na Pwani ya Magharibu. Ndipo kwa hakika tunahitaji maombi yenu, ili Mungu wa Mbinguni akatupe rehema kule na ibada kuu. Nilikuja tu jana au jana usiku hasa, nikichelewa na jana ilikuwa mojawapo ya, vema majuzi na jana ilikuwa mojawapo ya siku kuu maishani mwangu.

Ninajua, kuna hawa watu wawili au watatu humu jengoni ambao ni mashahidi wa kushuka Kwake Bwana jana na jambo kuu na la ajabu lililotukia, ambalo sina wakati wa kuwaambia asubuhi hii, bali huenda nikwaaambia Jumapili ijayo asubuhi, kabila ya kuondoka. Huenda—nikawa na wakati kwenye ujumbe ku—kuwaambieni. Kama Bwana anapenda nitakuja angalau kuwaombea wagonjwa Jumapili asubuhi . . .? Ninataka kuondoka yapata saa sita mchana ikiwezekana kwa mikutano ya San Jose. Katika San Jose, California. Na iwapo una watu wowote huko Pwani ya Magharibi, hiyo ni—tunaamini utaenda kuwa, labda wakati ambao nimeutazamia kwa muda mrefu, badilido katika huduma yangu ijayo. Na liko karibu sana. Nilidhani lilikuwa litendeke jana na, ah, ninaamini kwamba itakuwa moja kwa moja sasa na itakuwa zaidi ya kitu chochote ambacho tumewahi kuona au kusikia bado. Sasa kumbukeni hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Na kwa hivyo sisi twaitazamia wakati wowote. Na tutakuwa na mkutano sasa katika uwanja wa maonyesho, naamini hiyo ni sawa, sivyo, Gene? Katika uwanja wa maonyesho huko San Jose, California. Na utakuwa mkutano wa siku kumi kuanzia tarehe 20 hadi 29, a-ah, huko San Jose. Mimi—iweni tu mkitukumbuka na kutuombea. Sasa tuna yapata, kama tutatoka katika wasaa, yapata masaa, mawili na nusu sasa ambapo tutaenda ku a—ah, kuanza ibada zetu za kuwaombea wagonjwa na kulileta neno.

Basi nimechagua asubuhi hii fungu ndogo la Maandiko, mahali pawili katika Biblia, pa kuzungumzia. Lakini kabla hatujazungumuza, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mchache, kwa maombi.

2 Mungu mwenye neema nyingi sana, tunakikaribia kiti Chako cha neema kwa unyenyekevu asubuhi hii, kama watoto wasiostahili, lakini tukija na imani isiyoghoshiwa katika Mungu, tuliyopewa na Roho Mtakatifu, na Uwepo Wake wa daima pamoja nasi. Na katika ahadi kwa Bwana Yesu, ya kwamba tukija kwa unyenyekevu na kuomba cho chote katika Jina

Lake, tungepewa haja zetu. Kwa hivyo, hatuyatumaini matendo yetu mema, kwa sababu hatuna yo yote, kama hayo, bali tunautumainia ule ustahifu wa Kalvari, ambapo tulipewa neema yetu bure na Mwana wa Mungu. Nasi ni vigumu kutuliza majonzi ambayo yanatiririka makooni mwetu, tunapowazia ya kwamba sisi, watu wasiostahili, na jinsi ambavyo kwa neema Yake hapo Kalvari Yeye alitutenda hayo, tupate kuletwa karibu sana na Mungu, hata kufikia uhusiano. Na sasa sisi ni wana wa kiume na wa kike Kwake.

3 Nasi twaja asubuhi hii, Bwana, chini ya paa hili ndogo, kujiweka wakfu wenyewe, na kwa ibada, tukiungama dhambi zetu, na—na katika ibada ya Kiungu. Tunatumaini ya kwamba utakuwa pamoja nasi na utupe ufahamu wa kiroho wa kuja Kwako kunakokaribia, kusudi tupate kuitayarisha mioyo yetu kila siku kwa hilo tukio kuu lililotarajiwa kwa maelfu ya miaka. Bila shaka viumbe vyote vinaugua, vikilialia kuwekwa huru. Na roho zetu ndani yetu, Bwana, kila mara zinaungama ya kwamba "sisi ni wageni na wasafiri, na hapa si nyumbani kwetu, bali tunautafuta Mji Ambao Mwenye Kuubuni na Kuunjenga ni Mungu." Twautarajia wakati huo ulio mkuu kuja.

4 Bwana, tutakuwa waangalifu kwamba mikutano hii, tukutanikapo hapa, tutawaombea watoto Wako walio wagonjwa na wanaoteseka. Nasi tunaomba ya kwamba utakutana nasi leo katika njia maalum sana, kuponya magonjwa yote na maradhi kati yetu. Na huenda ikawa, Bwana, kuwa ahadi hii ambayo nimetangulia kunena juu yake, mkutanani pamoja nawe hapo jana, mara tu baada ya mapambazuko, na jinsi Wewe ulivyoithibitisha mara kwa mara tena. Nasi tunajisikia ya kwamba saa ile imekaribia sana. Hii na iwe siku ile, Bwana, ambapo itatendeka, upate kubadili huduma hii, Bwana, iwe kitu ambacho kitakuwa cha neema zaidi kwa watu Wako.

5 Na sasa, Baba, Mungu, hatuwaombei tu hawa hapa, bali wale wote walioenea kote duniani, walio na mahitaji ya kiroho na ya kimwili pia. Wape, Ee Bwana, ile shauku ya mioyo yao, kwa sababu watoto Wako wanajitahidi siku hizi. Udhalimu wa yule adui una nguvu sana, bali Wewe una nguvu saidi. Maana imeandikwa, "Aliye ndani yenu ni mkuu kuliko aliye ulimwenguni." Na kwa hili tunashinda. Nena nasi kwa Neno Lako lililoandikwa. Nasi tuondokapo asubuhi ya leo, na tusema kama wale waliotoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Twaomba katika Jina Lake Yesu aliyetupa ile ahadi. Amina.

6 Ninasoma sasa toka mahali pawili katika Kitabu cha Mwanzo, mojawapo panapatikana katika sura ya 24, kuanzia kifungu cha 56, husomeka hivi.

*Naye akawaambia, Msinikawishe, mradi BWANA amefanikisha njia yangu, nipeni ruhusa niende kwa bwana wangu.*

*Wakasema, Na tumuite huyo msichana, tumuulize mwenyewe.*

*Wakamwita Rebeka wakamuuliza, Je! utakwenda na mtu huyu? Akasema, Nitakwenda.*

*Ndipo wakampeleka Rebeka na ndu—ndugu yao, na yaya wake, na mtumishi wa Ibrahimu, . . .*

*Wakambariki Rebeka, wakamwambia, Ndugu yetu, uwe mama wa kumi elfu, mara elfu nyingi, na wazao wako waurithi mlango wa hao wawachukiao.*

7 Na katika Mwanzo 22, kifungu cha 15, twasoma.

*Malaika wa Mungu akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni,*

*Akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu, asema BWANA, kwa kuwa umetenda neno hili, . . . wala hu—hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee,*

*Katika kubariki nitakubariki, na katika kuzindisha natauzidisha uzo wako kama nyota za . . . Mbinguni, na kama mchanga . . . ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao;*

*Na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa kwa sababu umetii sauti yangu.*

8 Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Maneno Yake. Basi ningependa kuchukua, ikiwa laweza kuitwa fungu la maneno, somo langu asubuhi hii, kwanza, ni, *kujaribiwa mbele za malango yaliyoahidiwa*, nalo somo ni: *Kumiliki Malango Ya Adui.*

9 Mungu alikuwa akimjaribu yule mzee wetu kwa sababu Yeye alikuwa amempa ahadi. Na Mungu anapotoa ahadi, Yeye hutaka kuhakikisha kuwa mtu huyu anaistahili hiyo ahadi, kabla hajatimiza kile alichosema ama anachoahidi. Kwa hivyo Ibrahimu alikwisha kuahidiwa ya kwamba kupitia kwa uzao wake ulimwengu wote ungebarikiwa, ya kwamba angekuwa na mwana, naye huyu mwana, toka kwake atakuja Mzao ambaye angeibariki dunia nzima. Basi Ibrahimu, hiyo ahadi ilipotolewa kwake, alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano; naye Sara, mkewe, alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Lakini Biblia inatuambia kuwa Ibrahimu hakusita katika ahadi za Mungu, kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimsifu Mungu. Naye Mungu, mara kwa mara, alimjaribu, bali yeye alikuwa amefikia hilo jaribio la mwisho kabla ile baraka haijatokea.

10 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Uzao wote wa Ibrahimu. Mungu hutupa jaribio la mwisho kabla tu hajatupa ahadi. Na kama ingaliwezekana, ningetaka kusema jambo fulani hapa, langu binafsi, bali nitalizuia hilo. Jaribio hilo la mwisho, kuona jinsi utakavyofanya. Basi alipokwisha kumpa Ibrahimu jaribio hili, aliona kwamba Ibrahimu alikuwa mwaminifu tu kama alivyokuwa alipoanza. Ingekuwa baraka jinsi gani asubuhi hii kama sisi tunaopokea ahadi Yake ya uponyaji tungalikuwa waaminifu tu kama tulivyofanya tuliposimama hapa na kuipokea, haidhuru daktari alisema nini, tudumu tu tungali waaminifu.

11 Basi alipotenda hili na hakumzuilia mwanawe wa pekee, lakini alikuwa karibu kumchoma kisu Isaka kifuani, kuharibu ushuhuda wake . . . Yeye alikuwa ameshuhudia kote katika dunia iliyojulikana aliyoijua, ya kwamba angempata mtoto huyu. Kisha huyo mwana alipokuja, aliambiwa ageuke akalivunje lile tumaini pekee alilokuwa nalo kutimiliza ushuhuda wake. Basi Mungu alipoona ya kwamba yeye alikuwa mtiifu kwa ile imani aliyokuwa nayo katika Mungu, Mungu akatazama toka Mbinguni akasema, "Nimeapa kwa nafsi Yangu kwamba nitakubariki na kukuzidisha, na uzao wako utamiliki mlango wa adui wake." Ni ahadi jinsi gani!

12 Naye Rebeka, ambaye angekuwa mama ya huyu mwana mashuhuri, aliyeahidiwa, aliyengojewa, alipoitwa kwa jaribio la mwisho la mwanamume mgeni ambaye hakuwa amepata kumwona hapo mbeleni, ila yeye aliona tu matendo ya Roho Mtakatifu. Basi wazazi wake waliposhindwa kukata kauli kabisa kama yeye angeondoka na huyu mgeni au la, akawe mke wa mwanamume ambaye hakuwa amemwona, yeye aliletwa kwa lile jaribio la mwisho. "Tutamleta msichana na kumruhusu azungumze. Tutasikia toka kinywani mwake iwapo atakwenda, ndio au la."

13 Hivyo ndivyo linavyoletwa kwa Uzao wote wa Mungu. Sharti kiwe kinywa chako. Mungu anataka kusikia kutoka kwako.

14 Kwa hivyo yeye alipojaribiwa, hakusitasita hata dakika moja. Yeye alisema, "Nitakwenda." Napenda hilo. Sio, "Hebu ni kate shauri, hebu niyachunguze tena." Yeye alikuwa ameshawishika kabisa! Hao ndio watu Mungu anaweza kuwatumia, unaposhawishika kabisa ya kwamba Mungu atatimiza ahadi Yake. Kasema, "Nitakwenda!"

15 Nao watu wake basi walikuwa na upako sana, labda hawakujua, bali wao walitoa unabii walipoweka mikono yao juu ya dada yao, na binti yao, msichana mrembo wa Kiyahudi, walipokuwa wakimpandisha juu ya ngamia na kumpeleka katika nchi ya kigeni, kati ya watu wageni. Lakini kulikuwa na kitu fulani juu yao, wao walisema, "Na uzao wako waumiliki mlango wa adui wao. Uwe mama wa milioni elfu kadhaa."

16 Na leo huo ukoo wa watu na watu wa Mungu wanatangatanga kutoka bahari hadi bahari kote duniani. Katika ule ufufuo watakuwa kama nyota za Mbinguni, wakati hizo nuru zenye kuangaza zitakapochukua mahali pao, zinapopita angani. Nao watakapokuja watakuwa kama bahari karibu na . . . ama mchanga ufuoni mwa bahari. Watakuwa milioni elfu kadhaa.

17 "Uzao wako utamiliki mlango wa adui wake." Hiyo ni ahadi aliyoapa Mungu. Ule uzao wa Ibrahimu. Ndiposa kwa Roho Wake Mtakatifu, akiona ya kwamba yule mama angekuwa sehemu ya yule mwana pia, kwa sababu wao ni shemu ya ule mwili, basi Roho Mtakatifu akitenda kupitia kwa watu hawa, alisema, "Yeye . . . uzao wako utamiliki mlango wa adui." Kisha Mungu akiapa Yeye angemiliki mlango wa adui, basi hilo linaweka kanisa la Mungu aliye hai katika hali gani?

18 Sisi ni uzao wa Ibrahimu, kwa kuwa sisi tu wafu katika Kristo, ndivyo tulivyo, tunafanyika uzao wa Ibrahimu nasi tu warithi pamoja naye chini ya ahadi ile ile iliyoapiwa. Sisi tu uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi wa kila ahadi aliyopewa. Lakini, majaribio yajapo, hapo ndipo tunaposhindiwa. Bali siamini ya kwamba uzao wa kweli wa Ibrahimu utashindwa, wao watasimama kwa ushujaa na uaminifu kama alivyofanya Ibrahimu.

19 Sasa tunaona ya kuwa Mungu hawezi kusema cho chote au—au afanye ahadi yo yote isipokua tu awe ataitimiza. Yeye hana budi kufanya hivyo kusudi awe Mungu. Miaka kadha baadaye, wakati watu wawa hawa, watu walioahidiwa, yule mzao wa Ibrahimu alipokuwa safarini kwenda kwenye nchi ya—ya ahadi, kulikuwa na mlango ambaye alisimama, wima dhidi yake, naye alikuwa ni ndugu yake mwenyewe, Moabu, aliyesema, "Hutapitia nchini mwangu. Nitahakikisha ya kwamba haupitii nchini mwangu."

20 Yeye alisema, "Ng'ombe wetu wakila nyasi zozote zenu au kunywa maji yoyote yenu, tutawalipa kwa ajili yake."

Lakini yeye alisema, "Hamtapitia nchini humu."

21 Lakini ahadi ya Mungu ilidumu kweli. Kwa hivyo wao wakaenda wakamleta nabii wao, Balaamu, wakamleta kule chini apate kuwalaani watu hao. Na aliyosema ni haya. Wao walijaribu kumwonyesha sehemu iliyo baya sana ya huo uzao uliobarikiwa, bali Mungu akamwonyesha sehemu yao iliyo nzuri sana. Yeye alisema, "Ye yote atakayewalaani Israeli atalaaniwa, na yeyote atakayewabariki atabarikiwa." Na vizuizi vikaondoshwa na Israeli wakavuka nchi tambarare. Mungu alimwahihdi atamiliki mlango wa adui yake.

22 Miaka mingi baadaye, akatokea mtu jina lake Danieli, aliyekuwa wa ukoo wa Uzao wa kifalme, na wa ahadi zile, kwa kuwa alikuwa mzao wa Ibrahimu. Naye Mungu alikuwa amemchagua kabla ya kuwekwa misingi ya dunia,

awe nabii wake. Naye aliishi ali shujaa na mwaminifu, na hata katika nchi ya kigeni, yeye alikuwa amekusudia moyoni mwake, "Sitajichafua na wao." Huyo ndiye mzao halisi wa Ibrahimu. Akiishi katika nchi iliyo tofauti, akiishi kati ya watu walio tofauti, hata hivyo akiizingatia kwa dhati hiyo ahadi, "Sitajichafua na wao. Nitadumu mwaminifu."

23 Mungu alimjaribu kama alivyomfanyia baba yake, Ibrahimu. Naye mfalme akasema, "Aidha wewe utakuwa mmoja wetu uabudu tunavyoabudu, au nitakutupa katika tundu lililojaa simba wenye njaa."

24 Danieli, kama Ibrahimu, babaye, akasema, "Unaweza kunitupa katika tundu la simba, lakini sitasujudu yo yote ya sanamu zako. Sitaichukua dini yako baridi. Nitadumu mwaminifu kwa Yehova."

25 Basi pale pakaja maonyesho ya nguvu. Mfalme alitimiza ahadi yake na kumchukua yule nabii, au aliamuru achukuliwe akatupwe tunduni mwa simba. Na wakati hao simba, hao adui zake walipomkimbilia nabii, Mungu alitimiza ahadi Yake. Akamiliki mlango wa adui wake. Mungu alimsimamisha Malaika hapo mbele ya hao simba, akautwaa huo mlango.

Mungu hutimiza ahadi Zake, "Yeye atamiliki mlango wa adui wake!" Mungu alisema hivyo.

26 Kisha kulikuwa na watu wengine watatu huko walioahidi kwamba watakuwa waaminifu kwa jambo hilo, ambao kweli walikuwa uzao wa Ibrahimu, nao walikuwa Shadraka na Meshaki na Abednego, kisha wakatiwa jaribioni. Nao wakasema, "Msipopiga magoti mnaposikia zeze zikipigwa na tarumbeta zikilia, msiposujudu dini yetu, na kuyaacha mambo hayo mnayoya— mnayoyashikilia! Nanyi nyote mmelowa maji kwa vyo vyote, dini yenu haifai zaidi kuliko ya mtu mwingine." Je, hatusikii hayo wakati wote? Lakini ile—ile dini ya Yesu Kristo ni tofauti. Zile nguvu za kufufuka Kwake ni tofauti. Sisi tu watu tofauti, watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme. Mungu hutofautisha.

27 Lakini wasemapo, "Yakupasa uwe mmoja wetu!" Ingekuwa sawa kwa Shadraka na Mashaki na Abednego kama wangetaka kuwa mmoja wao, lakini hawangekuwa mmoja wa wale wageni. Sasa, wao walisema, "Msipofanya hivyo, tuna mlango nje hapa unaoelekea kwenye tanuru ambao tunaweza kuufungua na kuwatupeni humo, nanyi mtatamani mngelikuwa mmoja wetu."

28 Wao walikumbuka ile ahadi. Wao wakawapitisha moja kwa moja katika tanuru ya moto, nao walipoufungua ule mlango na kuwatumbukiza kwenye miali ya moto, maadui wao ambao wangeliwaangamiza, wao wakamiliki malango ya adui wao. Mungu alimtuma Mwanawe mle mialini mwa moto akaipoesha hiyo mivuke, naye akaongea pamoja nao walipokuwa mle ndani. Ahadi ya Mungu ikawa kweli. Wao wakamiliki mlango

wa adui. Wakajaribiwa kwanza, kisha wakamiliki mlango wa adui. Si ni Yesu aliyetoa ahadi, "Ukimuudhi mmoja wa hawa walio wadogo, ingekuwa heri kwako kama jiwe la kusagia lingelifungwa shingoni mwako ukazamishwe kwenye vilindi vya bahari. Usiwaudhi hawa wadogo wanaoniamini Mimi. Na ishara hizi zitafuatana na hao waniaminio Mimi."

29 Yeye aliwatofautisha. Yeye alionyesha wale walioamini na wale hawakuamini. Kila mara kuna makundi matatu ya watu, hayo ni, asiyeamini, anayejifanya mwamini, na mwamini. Lakini Mungu ana njia ya kuthibitisha ni nani aliye mwamini. Mwamini huyo huwa imara kwa yale Mungu asemayo kuwa ni Kweli. Ndiyo.

30 Ilikuwa Eliya, Mtibishi, alipofikia maonyesho ya nguvu hadi akadhani ndiye pekee taifani aliyekuwa akali anamwishia Mungu. Naye mfalme yule alikuwa amtie jaribioni, nao wakamtesa. Kisha huyo malkia aliyejipaka rangi aliyeitwa Yezebeli, akatisha kumuua. Basi alipofikia yale maonyesho ya nguvu, Eliya akamiliki milango ya adui yake na kulirudisha taifa lote kwa Mungu tena. Mungu hutimiza ahadi Yake.

31 Ilikuwa Musa, baada ya yeye pia kuwa katika huu uzao wa kifalme, ule uzao wa Ibrahimu, kwamba alipotumwa kwenda Misri kuwakomboa wana wa Israeli, naye Mungu alikuwa amempa kutenda ishara na maajabu, na kuipiga dunia, na kuwaagiza vyura na viroboto na giza na mvua ya mawe na mvua ya moto, naye alikuwa amefanya miujiza hii yote. Hata hivyo yeye alipowaongoza kuwatoa kwa mkono wa Yehova, ulifika wakati ambapo yeye alipokabiliana na mlango fulani kati yake na ile nchi ya ahadi, kulikuweko na bahari ya Shamu, kizuizi njiani. Walikuwa wamezingirwa na jeshi la Farao, milima na majangwa na Bahari ya Shamu, bali Musa alijitokeza na kuumiliki mlango wa adui yake, kisha akavuka ile Bahari ya Shamu kavu, kama kwamba alikuwa akitembea katika barabara yenye vumbi. "Mtamiliki mlango wa adui." Mungu alisema hivyo na hilo latosha!

32 Ilikuwa tu miaka michache baadaye wakati majaribu yalipokuja, na kanisa lote likatetemeka, kama ilivyo rahisi kwa kusanyiko la watu kufanya wakati jambo fulani halionekani likitendeka jinsi ipasavyo. Mungu hulifanya liwe hivyo. Mungu huleta mvutano kanisani, "Maana kila mwana ajaye kwa Mungu lazima ajaribiwe na athibitishwe, na ahakikishwe." Yeye huruhusu upatwe na ugonjwa. Yeye huachilia magonjwa yakujie, kukujaribu na kukuthibitisha, kuuonyesha ulimwengu ya kwamba wewe hakika u uzao wa Ibrahimu. Yeye huruhusu hayo kwa mapenzi Yake Mwenyewe. Yeye huruhusu msiba, huruhusu marafiki kuwa kinyume chako. Huruhusu mambo hayo yote, na kumwachilia Shetani akujaribu, naye atafanya yote ila kuutwaa uhai wako. Yeye angekutupa katika kitanda cha dhiki, angeruhusu jirani zako wakuchukie, angeruhusu kanisa

likuchukie, anaweza kufanya karibu kila kitu, na ni mapenzi ya Mungu Kwake kufanya hilo. Tunafundishwa lina dhamani zaidi kwetu kuliko dhahabu.

33 Vipi basi kwa Ibrahimu pamoja na Isaka, mlimani, yule ambaye alipewa ahadi, na kwa uaminifu wake na kujua kwake, na imani yake katika Yehova, ni kupitia kwa hiyo na hiyo pekee ambayo Mungu alitazama chini na kusema, "Uzao wake utamiliki ile milango. Nimeapa kwa Nafsi Yangu kuwa nitafanya mambo haya." Hamna mwingine aliye mkuu zaidi ambaye Yeye angeliapa kwake, bali akaapa kwa Nafsi Yake. Basi ikiwa Yeye alimwachilia Ibrahimu ajaribiwe hata hicho kiwango cha mwisho, hana budi kukujaribu wewe na mimi hadi hicho kiwango cha mwisho, huo wakati wa kukata kauli wakati kila kitu kimekuacha, yakupasa usimame peke yako hapo. Haleluya! Ndivyo hivyo.

34 Simama peke yako! Kwenda nje huko ukaseme, "Hata akiniva, bado nitamtumainia." Huo ndio uzao wa Ibrahimu. Huyo ndiye Yule anayetoa ahadi. Haidhuru wengine wao watasemaje, au wengine watatenda nini; "Mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Mungu," kasema . . . Wengine wao wakisema, "Hakuna lo lote katika hicho kituko, ni kuwashwa-washwa tu"; "mimi na nyumba yangu tutamtumikia Mungu!" Nami nataka kuungama na Paulo papa hapa, na kusema, "Kwa njia ile waiitayo 'uzushi' ndivyo ninavyo mwabudu Mungu wa baba zetu." Hata wawe wapayukaji kanisani, hata wawe walaghai, na hata wawe namna zote za manabii wa uongo, na kila kitu kanisani kati ya watu, na katika ujirani, kila kitu, bali mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana! Hata wote wakome kuja, hata kanisa lote liwe baridi, na kutojali; mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana! Hata ikiwa mtu fulani aliombewa wala hakupona, hilo si kitu; mimi na nyumba yangu, tunamtumikia Bwana! Kujaribiwa na majaribu.

35 Wanadamu sio wasiokosa, bali Mungu hakosei. Mwanadamu, ukiweka nia yako juu ya mwanadamu, yeye atafanya kosa. Labda si kwa kupenda, bali yeye atafanya hivyo. Mungu humruhusu afanye hivyo kusudi aitikise imani yako itoke kwa mwanadamu. Imani yetu haimo katika hekima ya mwanadamu, bali katika nguvu za ule ufufuo wa Yesu Kristo. Hapo ndipo ule uzao halisi wa Ibrahimu hupumzisha ahadi yao, kwa sababu wao wanaweza tu kuwa uzao wa Ibrahimu wanapompokea Roho Mtakatifu. Bila Roho Mtakatifu wao si uzao wa Ibrahimu. Na imani ile ile iliyokuwa katika Ibrahimu humjia mwamini. Haidhuru nini kitakachotendeka au ni kinyume vipi, mwamini husonga mbele moja kwa moja.

36 Wale wapelelezi walirudi na kusema, "Ee, ni, ni upuzi kujaribu. Hamna haja ya kuendelea mbele zaidi, kwa sababu hao watu ni majitu wakubwa mno huko, na wana serikali kuu,

nao—nao wana mikuki, na, kwani, sisi twaonekana kama panzi kando yao."

37 Sijui, bali nimeshawishika kuamini hapa kuwa Yoshua alikuwa mfupi wa kimo, mtu mdogo. Naweza kumwona akiruka juu au kitu kama sanduku, na kusema, "Waume na ndugu zanguni," na kwa watu milioni mbili, "sisi tu zaidi ya kuwamiliki wao!" Unaona? Kwa sababu gani? Hapo palikuwa uzao wa Ibrahimu. Mungu alitoa hiyo ahadi. Hiyo ilikuwa mali yao. Mungu alitoa hiyo ahadi. Haidhuru upinzani ulikuwaje, ule uzao halisi wa Ibrahimu ulisema, "Tutaitwaa kwa sababu Mungu alitupa!"

38 Mnasimama hapo asubuhi ya leo. Hapo ndipo Kanisa la Mungu aliye hai linaposimama. Sijali yale mtu ye yote asemayo, yale daktari asemayo, cho chote kile, yale asiyeamini asemayo, tunaweza kushinda zaidi cho chote kijacho. Sisi ni wazao wa Ibrahimu nasi tutamiliki mlango wa adui wetu. Haidhuru adui ni nini, Mungu alitoa ahadi! Hiyo ilikuwa yao, mali yao.

39 Uponyaji ni mali yako, wokovu ni mali yako. Roho Mtakatifu ni mali yako. Na kuna maelfu kadha ya wahubiri na wengineo nchini leo, wasemao, "Sivyo ilivyo." Lakini ule uzao wa Ibrahimu unajua ndivyo ilivyo. Wao hujiingiza ndani moja kwa moja na kumiliki milango ya adui. Mungu alisema wangefanya hivyo. Wao wanaamini hilo kwa sababu ni ahadi. "Uzao wake utamiliki milango ya adui." Naam, utapitia katika shida na majaribu.

40 Yoshua alisimama hapo mwaminifu. Huyo mtu mdogo akasema, "Sijali wao ni wakubwa vipi, sijali wao wana mkuki wa aina gani, miji yao imezungushiwa kuta ndefu vipi, na ni kuu vipi, ahadi yetu ni kwamba 'huo mlango utamilikiwa na ule uzao wa wana wa Mungu,' nasi tunaenda huko kuitwaa. Sisi tu zaidi ya washindaji kwao!" Lo, huyo ndiye mzao halisi.

41 Wengi wao waliozaliwa wakiwa mbegu ya kawaida, kasema, "Hatuwezi kufanya hivyo. Hakuna haja ya kujaribu. Kisha, sisi ni wachache kwao, wao ni watu bora zaidi, sisi tu kila kitu." Haidhuru, yeye hangeweza . . . Wao walikuwa wakitazama kile . . . kile jicho lilichoona, naye Yoshua alikuwa akitazama kile Mungu alichosema.

42 Ule uzao wa Ibrahimu hautazami yeyote ya mambo yale ya kawaida; wao hutazama kile alichosema Bwana. Hiyo ni ahadi. Ingekuwaje kama Ibrahimu angalitazama kilicho cha kawaida? Kumtazama mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja, alikuwa na miaka tisini, naye alikuwa na miaka mia, na alikuwa ameishi pamoja naye tangu alipokuwa msichana mdogo naye akiwa mvulana mdogo, na hamna uzao. Yeye hakuangalia mambo hayo. Alisema aliyahesabu mambo hayo kama kwamba hayakuwako, maana yeye alitazama yale aliyosema Mungu. "Nitakubariki, Ibrahimu, kisha nitakupa uzao kupitia Sara."

Naye akaamini. Hutazami upande wa upinzani; twatazama kile alichosema Mungu. Mungu alisema, hilo latosha!

43 Kwa hivyo basi walipofika huko Yordani, Yoshua alipofanywa amri jeshi, nao wakafika ukingoni mwa maji na wangetazama na kuuona Yeriko, lakini, kati yao, Yoshua alipolitayarisha jeshi lake, kulikuweko na mlango mmoja. Na mlango huo uliitwa Yordani. Lakini ahadi ya Mungu inafaa kwa kila mlango. Haidhuru mlango gani, ahadi ya Mungu inafaa. "Yeye atamiliki malango ya adui wake." Hilo latosha. Yeye alipofika Yordani asubuhi hiyo, labda, nitaamini ya kwamba Shetani alikuwa na wingu la dhoruba huku likining'inia kila mahali, yale maji mengi ya kale yenye matope yakitapakaa chini, mashamba yalijawa na mafuriko. Lo, ni wakati wa majaribu jinsi gani! Lakini Yoshua alisema, "Iweni tayari, mtauona utukufu wa Mungu!" Nao wakajitakasa na wakawa tayari, wakajitayarisha wakati kila kitu kilionekana kinyume. Lakini huo ulikuwa uzao wa Ibrahimu, ambao Mungu aliwaapia, "Nitawapa ule mlango." Yeye alifika Yordani, ambao ulikuwa mlango wake, kisha akaumiliki.

44 Mojawapo ya asubuhi hizi sina budi kuufikia mlango huo wa mwisho. Huna budi kuufikia Yordani, lakini yule mzao wa Ibrahimu ataumiliki huo mlango. Haidhuru ni nini, ataumiliki mlango wa kila adui.

45 Watu hao walikuwa wakuu, wao walikufa mmoja baada ya mwingine. Lakini hatimaye siku moja katika Bethlehemu ya Yuda, yule Mzao wa Kifalme akazaliwa, ambapo wengine wao wote walikuwa tu vivuli. Yule Mzao wa Kifalme alizaliwa, si kutokana na mwanamume, bali Yeye alizaliwa na bikira, akiwa na ile Nguvu mishipani Mwake ya kushinda mauti na kuzimu. Mungu alitoa ahadi. Mwanadamu wa kawaida hangeweza kufanya hivyo. Bali Mungu anapotoa ahadi, Yeye ndiye Mungu yule yule aliyekuwa dakika chache hapo kabla pamoja na Ibrahimu, Yehova-yire, Bwana ataandaa njia ya kumiliki mlango. Tutafanya hivyo vipi? Yoshua alikufa, Musa alikufa, wengine wote walikufa, lakini Mungu alisema, "Yeye atamiliki mlango wa adui wake." Atamilikije mauti? Yeye ana njia ya kufanya mambo. "Yeye atamiliki mlango wa adui wake."

46 Yule Mzao wa kifalme alizaliwa. Yeye alijaribiwa kwa kila hali kama sisi. Kama tu vile wewe upaswavyo kujaribiwa vivyo hivyo Naye. Shetani alimchukua upesi Yeye alipompokea Roho Mtakatifu, nyikani kwa siku arobaini mchana na usiku, apate kujaribiwa. Naye alipotoka huko . . . Na katika kifo Chake, wao walipompigilia misumari mikononi, na kumtemea mate usoni Mwake. Yeye alipitia katika kila ugonjwa. Lakini yeye alipokuwa hapa duniani, alithibitisha kuwa yeye angeshinda magonjwa. Wakati mama ya mkewe Petro alipolala hajiwezi, kwa kupooza, yeye alimgusa mkono wake kisha hayo maradhi

yakamtoka. Yule mwenye ukoma alipolilia mlangoni, "Mchafu! Mchafu! Ukitaka, unaweza kunifanya mzima."

47 Yeye alisema, "Nataka. Uwe mzima." Yeye alishinda na akautwaa mlango wa ukoma. Yeye alichukua mlango wa homa kali. Yeye alifanya kila maumbile yamtii. Yeye alikuwa Yule Mzao wa Ibrahimu, yule Mzao wa Kifalme, yule ambaye alipewa ile ahadi, kupitia Kwake Ibrahimu na uzao wote uliomfuata hadi kwa yule Mzao wa Kifalme na uzao wote baada Yake. Ahadi ya Mungu ni kweli. Yeye alishinda magonjwa. Alishinda majaribu. Adui alipomtemea mate usoni, akampiga shavuni, Yeye alimgeuzia upande wa pili. Walipong'oa ndevu kidevuni Mwake na kumtemea mate, Yeye hakulipiza kisasi. Yeye alishinda mlango wa majaribu na kuumiliki.

48 Ndipo wasema, "Hasira yangu haitaniacha nitende vile." Nawe ni uzao wa Ibrahimu, naam, bwana, Yeye alikushindia.

49 Naye alipodhihakiwa, hakudhihaki pia. Alipofanyiwa mzaha, alinyamaza. Alipoitwa Ibilisi, alinyamaza. Yeye alikuwa na wajibu moja, na hiyo ni kazi ya Baba, naye alienda kote akitenda hiyo. Kisha hatimaye wakampeleka mtini. Ilibidi mauti kumkabili. Hao wengine wote walikuwa wameshinda bahari, walikuwa wameshinda maumbile, na waliisha washinda simba, waliisha ushinda moto, waliisha shinda kila kitu ila mauti. Lakini kulikuwa na pigo moja ubongoni Mwake, mishipani mwake, nao walikuwa na nguvu ishindayo mauti. Kwa hivyo wakachukua mikono Yake na kumnyosha na kumpigilia misumari msalabani. Wao walimpiga na kumvua nguo hadi mifupa Yake ikamkodolea macho. Lakini Yeye alipofanya hivyo, nao walikuwa wamefanya kila walichoweza kutenda, mauti ikampiga, kasema, "Sasa nitakutwaa wewe jinsi nilivyomtwaa Yoshua. Nitakutwaa kama nilivyomtwaa Danieli. Nami nitatenda haya yote kwa kuwa nitakufanya ufe."

50 Naye alikufa hata jua likajionea aibu lenyewe. Alikufa mpaka maumbile yakaona aibu kisha yakashindwa kutenda kazi. Jua likatua wakati wa adhuhuri, nazo nyota hazikutokea. Yeye alikufa hata viumbe vya asili vikawa vyeusi sana hata hungeuona mkono wako mbele yako adhuhuri. Nadhani maumbile yalisema, "Hebu nife pamoja Naye."

51 Lakini, ndugu, ndipo Shetani alipeleka nafsi Yake ya thamani katika mashimo ya Jehanum. Hapo milango ikafunguka, bali Yeye alitoka humo siku ya tatu, aliishinda. Amina. "Uzao wake utamiliki mlango wa adui." Kashinda mauti, akashinda jehanum, hiyo asubuhi ya kwanza ya Pasaka alishinda mauti. Na sasa tunasimama tukiwa zaidi ya washindi, kupitia Kwake Yeye aliyetupenda.

52 Katika siku ya Pentekoste Yeye alimtuma Roho Mtakatifu aendelee kupitia kwa Mataifa, kuchukua uzao wa ahadi, kuwapa Mataifa, waliotupwa nje, kuwapa ubatizo wa Roho

Mtakatifu, apate kuwaingiza katika ile Ahadi. Sasa, tuna haki ya kushinda magonjwa yote. Haitubidi tuyashinde, yamekwisha shindwa. Inatupasa tu kudai ahadi na kuondoka kuitwaa. Tayari yameshindwa. Mauti yameshindwa, jehanum kumeshindwa, magonjwa yameshindwa, majaribu yameshindwa, pepo wote wameshindwa, jehanum kumeshindwa, mauti yameshindwa, kaburi limeshindwa. Tunasimama mlangoni, tukiuchukua! Hatuhitajiki kupiga raisasi. Imekwishalipiwa tayari.

53 Adui yake, Yeye atamiliki mlango wa adui yake. Ni maelfu ya mamilioni wangapi? Yeye atamiliki mlango wa adui yake, kila adui! Yeye alifufuka toka kwa wafu. Nasi tunaimiliki kwa sababu Yeye alitupa sisi. Yote ni kipawa cha bure, na zaidi ya hayo yote, na kila kitu ambacho Yeye ametenda, na kushinda kila mlango, Yeye alishinda magonjwa akaumiliki mlango ule. Jambo pekee litupasalo kutenda ni kutembea hadi mlangoni na kusema, "Katika Jina la Yesu Kristo, aliye Mshindi!" Amina.

54 Ifikapo wakati wa kufa, nayo mauti iseme, "Ngoja uone nikimfanya aikane dini yake."

55 "Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, rudi nyuma, ewe Yordani!" Ule uzao wa Ibrahimu huutwaa mlango ule.

56 Kwani, Paulo alisema, walipokuwa wakitayarisha kukikata kichwa chake, mzao wa Ibrahimu, yeye alisema, "'Uwapi, Ewe mauti, uchungu wako? Ku wapi, Ewe kaburi kushinda kwako?' Mungu ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

57 Yeye atamiliki mlango wa adui yake, kuutwaa! Sasa, Yeye hapigiwi mlangoni; ataushinda na kuutwaa, ataimiliki! Hiyo ni katika nguvu Zake Mwenyewe.

58 Katika Kanisa la Mungu aliye hai, asubuhi ya leo, kuna nguvu ya kuponya magonjwa yote. Katika Kanisa la Mungu aliye hai mna nguvu ya kushinda majaribu yote. Katika milki ya Kanisa la Mungu aliye hai, asubuhi ya leo, mna nguvu ya kugeuza dhambi na kuiondoa, na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika Kanisa la Yesu Kristo. "Lo lote mtakalo, ombeni katika Jina Langu nanyi mtapewa. Bado kitambo kidogo na ulimwengu (hao si ule Uzao, hao ni ule uzao usiozaliwa mara ya pili) hautaniona tena. Bali ninyi mtaniona, maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Ni nini? Ule Mzao wa Kifalme. "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Nitathibitisha kuwa Mimi niko pamoja nanyi, maana ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Yeye atamiliki uzao wa adui yake. Atamiliki, "uzao wake utamiliki mlango wa adui yake." Haidhuru ni nini kilicho mlango, ikiwa ni magonjwa, majaribu, dhambi, chochote kilicho mlango, umeshindwa tayari. Na ule uzao wa Ibrahimu utamiliki.

59 Je, huna furaha asubuhi ya leo kujua kuwa tunasimama sasa tukiwa zaidi ya mshindi, zaidi ya mshindi! Loo, hakuna

cha kupigania. Vita vimekwisha, filimbi imepigwa, Bendera imeinuliwa; na katikati ya kila tita la dhambi, katikati ya kila chumba cha wagonjwa, kuna ule msalaba unaoparuza uliosimamishwa kwa Damu ya Yesu Kristo, aliye Mshindi. Jambo pekee tunalofanya ni kuamini, tazama uishi. "Nitakuwa pamoja nanyi, nitathibitisha! Watu watakuja katika siku za mwisho, na kusema, 'Naam, vema, hayo *yalikuwa*.' Lakini nitakuwa pamoja nanyi, na kila jambo nililotenda hapa duniani, nitakuwa ndani yenu nikitendawatajo lile lile. Ndipo wao wata] ua. Wataniona Mimi. Wale. . . watu wa Wangu wataniona Mimi. Ule uzao wa Ibrahimu utaniona Mimi. Watanijua Mimi, watanitambua Mimi. Hao wengine wataniita 'Beelzebuli' kama tu vile wamekwisha kufanya, lakini mtanijua Mimi kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi. Mtaniona Mimi, kuona kwa macho yenu. Mtaniona Mimi, maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari. Jambo lile lile nitendalo Mimi, yeye aniaminiye kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya. Kazi za aina ile ile!"

60 Na siku hizi Kanisa la Mungu aliye hai lina heshima ya kusimama na kumwona Yesu Kristo ashindaye, aliyefufuka, Mwana wa Mungu aliye hai, akisimama sasa, akiishi katika Kanisa Lake, akitenda tena jambo lile lile alilotenda. Basi tunamiliki mlango wa kila adui.

61 Kama una adui asubuhi ya leo, basi, ndugu yangu, hakuna. . . kama wewe u mzao wa Ibrahimu, baada ya kusikia hili, hamna pepo wa kutosha jehanum wawezao kuuweka mlango huo mbele zako. Utafunguka. Sijali ni nini, utakwenda huko kama mzao aliyeahidiwa, useme, "Nadai hii kwa ajili yangu. Huu ni wangu kwa sababu Mungu aliapa kwamba atamfufua Yesu na katika Yesu nitaushinda, nami naja katika Jina la Mshindi huyo, Yesu Kristo. Simile, ninapita!" Amina. "Yeye atamiliki mlango wa adui." Basi, simama hapo wima mabega yako nyuma na ngao yako iking'aa, huku imeshafunikwa kwa ile Damu ya Bwana Yesu, yule adui ataitambua.

62 Ukiwa na haja, nena naye sasa tunapoomba. Nanyi mlio humu ndani asubuhi ya leo, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na ikiwa una haja, inua mkono wako kumwelekea Yesu kisha uinene moyoni mwako. Moyoni mwako, ukaseme, "Bwana, unaijua haja yangu. Sasa nimesikia asubuhi hii, na hiyo ni Biblia, 'Yeye atamiliki mlango wa adui.' Naja kuumiliki huo mlango. Labda nina hasira, labda nahitaji Roho Mtakatifu, dhambi imenifunga. Nina haja, lakini naja mlangoni sasa." "Nitautwaa asubuhi ya leo, mlango wangu. Kwa hivyo simile, napita."

63 Bwana aliye mbarikiwa, umeiona mikono hii yote, nawe wajua kuwa hili ni Neno Lako, Bwana. Nimelinukuu tu na kulieleza kote Maandikoni, wale watu wa Biblia, jinsi walivyoshinda falme na kutenda haki, na kuuzima moto, ukali

wa moto, na kuuepa ukali wa upanga, na kuvifunga vinywa vya simba, na, lo, wanawake wao wazee waliwapokea wafu wao waliofufuliwa, na mambo mengi kwa sababu Wewe uliahidi. Ni ahadi Yako, "Uzao wake, uzao wako, Ibrahimu, utamiliki mlango wa—wa adui." Nawe huitimiza ahadi Yako.

64 Sasa wape, Bwana, haja ya mioyo yao. Na waondoke hapa wakiwa watu tofauti. Na waende, wakijua wao ni—wao ni washindi kwa kuwa Yule Mzao wa Kifalme alishinda kwa ajili yao. Yule Mfalme wa fahari alipokuja, aliyezaliwa na bikira, Yeye alimshinda kila adui, hata mauti, kwa hivyo mauti yenyewe hayawezi kuutisha ule uzao wa Ibrahimu. Tuna ahadi ya kwamba tutarithi nchi, na tutarudi tena katika hali iliyo na utukufu zaidi, katika mwili uliotukuzwa, baada ya yule adui wa mwisho kuwekwa chini ya miguu, ya yule mwana wa pekee na wa mwisho wa Mungu atakayeingia katika ule Ufalme.

65 Iwapo kuna wale walioinua mikono yao juu, Bwana, ambao ni wenye dhambi, waokoe. Wale wanaoanguka, na wajue haiwapasi kubaki wameanguka. Yeye aweza kumiliki mlango huo wa kuanguka. Labda huyo aliye na hasira au u—ulimi mchafu, unaonena maovu, au roho yenye tamaa za kimwili, au anayetamani pesa au—au vitu vichafu, hebu na wajue ya kwamba wanaweza kumiliki mlango huo. Labda ni magonjwa, Bwana, mateso, wao wanaweza kuumiliki huo mlango, "Kwa maana alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichumbuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Sisi tu washindi asubuhi ya leo. Tujalie, Bwana. Na zaidi ya hayo yote, ile kazi kuu iliyofanywa naye, bali Yeye yu pamoja nasi. Hata hivyo Yeye aliahidi angeifanya. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa sababu nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Naomba, Baba, kuwa utajijulisha Mwenyewe kwa kila mmoja asubuhi hii. Maana twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

66 Je, mnaamini hayo kuwa Kweli? Amini kwa kicho kuwa ni Kweli, pasipo tashwishi hata kidogo moyoni mwako. Sasa kumbuka tu hili, kutenda kwa Roho Mtakatifu ni rahisi sana hata hutatanisha mwenye akili. Mambo rahisi sana ambayo nimewahi. . . Nimemwona Roho Mtakatifu akitenda hili; ningesema mambo ambayo, kwani, singewazia kwamba yangalikuwa hivyo. Ningalitumia akili yangu binafsi, ningesema, "Vema, hilo halingekuwa sahihi." Lakini kila mara ni sahihi. Yeye hutenda mambo kwa urahisi sana. Naye hutenda mambo kusudi ajijulishe Mwenyewe kwa watu Wake. Mungu yu pamoja na watu Wake. Yeye yu kati ya watu Wake. Yeye anawapenda na anataka kuwatumikia, na kuwasaidia, na kuwaruhusu wao wajue si yale atakayotenda, bali Yeye amekwisha tenda. Yeye tayari amelitenda, ni lako. Ni mali

yako. Ni kipawa cha bure kutoka kwa Mungu Baba yetu, kwa Kanisa Lake.

67 Sasa jinsi gani mawazo ya akili yatapotoshwa sana, kama katika siku za Danieli, na katika zile siku za wana wa Kiebrania, na wengi ambao habari zao tumezungumza juu yake asubuhi ya leo. Mnaona, ulimwengu mkuu wa kiakili wa siku hizo ulikuwa mgumu kushinda kama ulivyo sasa. Kila mara imekuwa ni adui, jinsi wao walivyoona na sayansi yao ya kisasa na mengineyo, ulikuwa tu wa kutatanisha na kadhalika kwa akili wakati huo kama wetu ulivyo leo. Unaona, lilikuwa jambo lile lile. Bali kulikuweko na wale, kila mara, waliothubutu kukaa hapo na kusema, "Mungu ni wa Kweli. Neno la Mungu ni Kweli."

68 Nawe, huhitajiwi kushinda, kwa sababu Yeye alishinda. Jambo pekee likupasalo kutenda ni kwenda tu na kutwaa, usimame mlangoni, useme, "Ni wangu. Huu ni wangu. Mungu alinipa, wokovu wangu. Nikitaka Roho Mtakatifu, Mungu alinipa. Ahadi ni kwa ajili yangu, kwa watoto wetu, wote walio mbali, na kwa wote watakoitwa na Bwana Mungu wamjie." Hiyo ndiyo sababu nasimama tu . . .

69 Huduma yangu ya huku kupambanua na kadhalika, itakoma hivi punde sasa. Lakini kila mara itakuweko, lakini punde si punde itakoma kwa sababu kutakuwako na kitu fulani kikuu zaidi. Mnaona? Inazidi kuwa kuu; toka kule kuutwaa mkono, hata upambanuzi, na sasa Yeye anajitayarisha kufanya lingine. Mnaona? Mnaona hilo? Lingojeeni mpate kujua ni kweli. Mwaona, najua ni kweli, na litaendelea kuwa kuu zaidi; la hali ya juu zaidi, bora zaidi. Bila shaka. Kwani Yeye aliahidi; na anachoahidi, Yeye hukitimiza. Yeye hawezi kushindwa katika ahadi Zake. Na ni nini? Uwepo Wake hudumu daima pamoja nasi, kuweka . . . kukufanya ujue kuwa Yeye amekwisha kuutwaa mlango kwa ajili yako.

70 Yeye alikuwa Mzao wa Kifalme, hamna ye yote aliweza kuitwaa milango hiyo ila Yeye. Hao wote kule nyuma walikuwa vivuli vya kuja Kwake, bali Yeye alipokuja hiyo ilimaliza vita vyote. Vita vyote viliishia huko Gethsemane na huko Kalvari. Na sasa tunasimama tu kama washindi. Mwaona, hakuna kufanya vita. Kwetu, vita vimekwisha, tunamiliki tu. Hati ya umilikaji wake, hakikisho liloandikwa na Mungu, Baba yetu, Yule aliyeuinua mkono Wake, kasema, "Naapa kwa nafsi Yangu kuwa Uzao wake utamiliki mlango wa adui." Na ndio huo, umekwisha kutwaliwa. "Alijeruhiwa kwa uovu wetu, kwa kupigwa Kwake tulipata kuponywa." Imekwisha tendwa. Kazi iliyomalizika, sisi tunaumiliki tu. "Na kazi nizifanyazo, nanyi pia mtazifanya." Yule Mfalme yu pamoja nasi asubuhi ya leo. Baraka Zake kuu, Roho Mtakatifu akitembea juu yetu. Kusikia hali hiyo ya utukufu, kujua inaambatana hasa na . . . inalingana na Neno la Mungu, inatupa faraja kuu sana kujua kuwa—kuwa Mungu ni Baba Yetu.

71 Sasa, naamini, je, yeye—yeye alitoa kadi za maombi asubuhi ya leo? Nilimwambia i—iwapo hakutakuwako na watu wengine isipokuwa wa Maskani hapa, vema, asitoe kadi zo zote za maombi, bali iwapo wa—wangekuweko yapata watu kumi, kumi na watano, au kitu kama hicho, wageni mlangoni, kwani, awape kadi za maombi, ili tupate kuwaleta humu tuwaombee. Ni wangapi walio wageni kwetu asubuhi hii, inua mkono wako? Lo jamani, hakika, wao ni kumi na watano ama ishirini. Vema. Tutapanga hizi kadi za maombi kisha tuwalete jukwaani. Mnaona, sababu ya kunena juu ya watu wa Maskani haya, wao wako hapo.

72 Huu upambanuzi, kumbukeni. Ninasema hili, huu upambanuzi hivi punde utakwisha. Kutakuwepo na kitu fulani kikuu zaidi na bora zaidi, hivi karibuni. Kulikuwako, nijuavyo mimi, mnaona, nawatazama ndugu wawili sasa waliokuwa wamesimama pamoja nami jana hilo lilipotendeka, mnaona, na hivi majuzi lilipotendeka. Na hiyo ni mara tatu mfululizo sasa limetendeka. Thibitisho kuwa liko karibu sasa, mnaona, linakaribia kutendeka.

73 Sasa, Bwana, Wewe ni Mungu, nasi tu watumishi Wako. Tunakushukuru kwa ajili ya Neno Lako, kwa ajili ya Roho Mtakatifu aliyebariki mioyo yetu. Na sasa tuna furaha, tumeketi hapa, tukijua ya kwamba sisi tu washindi. Sisi tayari tunamiliki milango yote ya adui. Imetolewa kwetu, nasi tunao ufunguo maalum mikononi mwetu. Jina la Yesu Kristo litafungua kila mlango wa adui. Chukua ufunguo huu, ule ufunguo wa Jina la Yesu, na ufungue kila mlango wa adui ambao umekufungilia mbali na ahadi yo yote. Na, Mungu, asubuhi ya leo tunakuja katika Jina la Yesu, na ufunguo huu, kuwafungulia milanga wagonjwa na wanaoteseka. Maana imeandikwa katika—katika Neno Lako, "Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Nao wakishika nyoka au wakinywa kitu cha kufisha, hakipaswi kuwadhuru. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya." Tunajua mambo hayo ni kweli. Na tujalie asubuhi ya leo, Bwana, kuwa wao hata, watu wataweza kuona hayo kupitia kwa dhihirisho la Neno likifanyika mwili na kuishi kati yetu, ya kwamba Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa, hebu walikubali na waponywe asubuhi hii, toka kwa magonjwa yao yote na maradhi na shida. Twaomba katika Jina La Yesu. Amina.

74 Teddy, waweza kupiga, *"Amini Tu,"* kwa utulivu na upole ukiweza. Na sasa mnataka nianze moja? Namba moja, kadi ya maombi. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, na kumi, au yo yote aliyoko. Vema. Mngeweza kwa utulivu mkiweza kusimama, njoni upande huu. A-ha? Karibu, hebu tuone, namba moja, namba mbili. Ni nani mwenye kadi ya maombi namba moja? A-ha? Namba mbili? Vema, Bwana. Namba tatu, namba

nne, namba tano, namba sita, namba saba, namba nane, namba tisa, namba kumi.

75 Huku wanapokuja na kuchukua nafasi zao za kusimama, ningetaka kuwauliza wengine wenu swali. Ni wangapi . . . Kuna mtu ye yote wa Maskani haya hapa aliye mgonjwa? Watu wa Maskani, inueni mikono yenu. Karibu mitano, minne, mitano, sita, saba, minane, mikono minane ama tisa. Je, kuna mtu humu Maskanini asiye wa Maskani haya, aliye mgeni kwetu, hata ingawa uliingia baada ya ibada na hukupata kadi ya maombi, je, unaweza kuinua mkono wako? Mtu ye yote aliye na haja na Mungu, ambaye bado . . . ambaye haji kwa Maskani haya. Mtu ye yote hapa asiye mshiriki wa Maskani haya, na—na hata hivyo u mgonjwa wala huna kadi ya maombi, waweza kuinua mkono wako, kila mtu? Vema. Ni nzuri. Sawa.

76 Sasa, nawasihi ninyi mwe na kicho sana mwezavyo kwa tu—tu dakika chache, kisha tutaanza mara moja na kuanza. Sasa hebu tuone, una nafasi kubwa vipi hapo, Billy? Vema, si hiyo . . . una namba kumi hapo? Niliita moja hadi kumi. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, tano, hebu wasimama sasa. Ikiwa wao ni namba kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, hebu hao wasimame. Sawa, moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili. Wamekosekana kama wawili zaidi, toka moja hadi kumi na tano. [Ndugu Branham anahesabu kimoyo-moyo—Mh.] Kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa na ishirini.

77 Lo, ngoja kidogo. Ni—nilimwambia atoe tu kadi za maombi kwa watu wasio wa Maskani. Vema, unaona, kwa sababu ingekuwa, unaona, upambanuzi. Watu husema, "Watu hawa huja kwenye Maskani." Mnaona, na—nawaambieni ni wangapi wamekuweko hapa, hawajawahi kuwa hapa hapo mbeleni, hebu tuone mikono yenu. Hamna mtu ambaye amewahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo mbeleni. Sasa, vema, hebu kidogo sasa, Ndugu Teddy.

78 Sasa, huenda nikasema hili, ya kwamba ninyi nyote ambao mmesikia mikutano, jinsi inavyoendelea, hata hivyo, mmesikia? Je, watu wote wamekuwa mikutanoni? Waona, Bwana wetu Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye hakudai kuwa mponyaji. Yeye alikuwa mzao wa Ibrahimu, bila shaka, naye alikuwa na ile ahadi. Alisema hakutenda neno hadi Baba amwonyeshe. Sivyo? Naye alisema, "Siwezi kutenda neno ila Baba anionyeshe la kutenda." Naye aliliona vema. Sio "Hadi Baba *aniambie* Mimi"; "hadi Baba *anionyeshe* Mimi." Yohana Mt 5:19, "Ninalomwona Baba akitenda, ndilo analolitenda Mwana vile vile."

79 Sasa wakati Yeye—Yeye alipokuja, tunaona ya kwamba mwanzoni mwa huduma Yake, ya kwamba baada ya Yeye kuchukua kile—kile kiti cha enzi cha Daudi . . . [Nafasi tupu

kwenye ukanda—Mh.] . . . kunena kiroho, wakati Roho Mtakatifu alipomjia hapo kwenye ubatizo wa Yohana, naye akawa Masihi mwenye upako. Sasa, kumbuka, Yeye alikuwa Mwana wa Mungu alipozaliwa. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira. Lakini Yeye alipokuwa Masihi, hapo ndipo Roho Mtakatifu alipomjilia, kwa sababu *Masihi* maana yake ni yule "aliye na upako." Mwaona? Naye alikuwa Aliye na Upako wakati Roho Mtakatifu alipomjilia. Mlinisikia nikihubiri juu ya *Mwana-Kondoo na Hua*. Ndipo tunaona ya kwamba Yeye . . . Baada ya siku arobaini za kujaribiwa Kwake, akatoka.

80 Na je, huduma Yake ilianzaje, na ilimalizikaje? Twaona kwamba katika huduma yake kulikuweko mtu mmoja jina lake Andrea, aliyekwenda akampata nduguye, Simoni, mvuvi, akamleta kwa Yesu. Basi Yesu akamwambia, akasema, "Jina lako ni Simon. Jina la baba yako ni Yona. Tangu leo utaitwa *Petro*, ambalo maana yake ni jiwe dogo." Mnakumbuka hilo? Naye mtu huyu akashangazwa na yale Yesu aliyomwambia! Sasa je, Masihi alipaswa kutenda hayo? Ni wangapi wanaojua hayo, semeni "Amina." [Kusanyiko lasema, "Amina"—Mh.] Ilimbidi awe Mungu-nabii. Naam, bwana. Musa alisema, "Bwana Mungu atawaondokeshea nabii kama nilivyo mimi. Na itakuwa ya kwamba ye yote asiyemskiza Nabii huyu atakatiliwa mbali na watu."

81 Sasa, kisha tunaona baadaye, Yeye alikuwa . . . Yeye alikuja kwa walio Wake. Hao ni akina nani? Wayahudi, kwa kimwili. Na kwa hivyo walio wake hawakumpokea, kwa hivyo ilimpasa basi . . . sasa Yeye anapaswa kuwaendea Mataifa, mnaona, kwa sababu wale walio Wake hawakumpokea. "Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Kwa hivyo sasa Yeye amewageukia Mataifa, na imekuwa hivyo kwa miaka elfu mbili. Lakini sasa tazama mambo aliyofanya.

82 Ndipo Filipo, baada ya kumwona akitenda hili, aliondoka akampata Nathanieli na kumwambia Nathanieli amemuona nani, na yale alikuwa ametenda, na hilo likamshangaza. Ilikuwa vigumu kuamini, bali yeye alipoenda Uweponi mwa Bwana Yesu, alipopata mahali alipokuwa, akaja Uweponi Mwake, Yesu alisema, "Tazama Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake."

83 Sasa, kama ungalikuwa umesimama pale, je, unadhani ungalikuwa wa kiroho kutosha kufahamu Yeye alikuwa nani? Je, unafikiri ingelifanya hivyo? Tazama sasa. Unaona, mtu huyo, mgeni tu, hapo huenda ikawa alikuwa mvuvi. Yeye alikuwa seremala, ndivyo alivyokuwa. Huyu seremala akisimama hapo, mtu wa makamu, kisha huyu mtu akaja. Akamtazama, kama mmoja wa watu hawa hapa, akasema, "Tazama Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake." Vema angalijuaje yeye alikuwa Mwisraeli? Si jinsi alivyovalia kwa sababu wote huvalia sawa.

"Hamna hila ndani yake." Yeye alijuaje alikuwa mtu a—asiye na hila?

84 Kwa hivyo ilimshangaza mtu huyu, akiwa mwamini halisi, alisema, "Rabi," au ndugu, mhubiri, mwalimu, "Uliniona lini?" Unaona, yeye alikuwa akimswali.

85 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona." Akasema, "Wewe u Mwana wa Mungu. Wewe u Mfalme wa Israeli."

86 Yesu akasema, "Kwa sababu nimekwambia hili, sasa unaniamini, sasa utaona mambo makuu kuliko haya."

87 Na hiyo ndiyo sababu naamini ya kwamba Kanisa la Mungu aliye hai litaona mambo makuu kuliko haya. Linakaribia kuingia katika hayo sasa, hivi karibuni, mnaona, kwa sababu wameamini. Wale waliolikataa kwa sababu ya vizuizi vya kidhehebu, nina shaka ikiwa wataamini cho chote. Mnaona? Mambo. . . Au utatembea Nuruni au utakuwa kipofu. Nuru hupofusha, au huonyesha njia.

88 Ndege wadogo, niliwapata, ilikuwa huko kwenye Sanamu ya Uhuru (hakikisha umewaona hao, ndugu Toms, utakapoenda huko, unaona), walipigapiga ubongo wao huko hata ukatoka. Nami nilisema, "Kuna nini?"

89 Nilisema, "Badala ya kufuata nuru, katika dhoruba, hadi usalamani, wao walijaribu kuigonga hiyo nuru, nao wakajiua."

90 Hilo ndilo jambo pekee linalotendeka unapojigongesha Nuru, utajiva, kiroho. Enendeni Nuruni kama Yeye alivyo katika Nuru, ndipo tutashirikiana sisi kwa sisi, makanisa yote yataamini na kuendelea kufurahia baraka za Mungu. Je, si hilo lingekuwa jambo la ajabu?

91 Mtazame huyo Mwanamke Msamaria alipokuja. Yeye alikuwa Msamaria, sasa; si Myahudi, Msamaria. Basi akasema, "Nipe maji ninywe." Na mazungumzo yakaendelea. Hili ni kwa walio wapya sasa. Na mazungumzo yakaendelea.

92 Sasa, mwanamke huyo hakujua Yeye alikuwa Masihi. Yeye alikuwa tu Mwa—Mwanamume, Myahudi. Tazama jinsi yeye alivyosema hapo kwanza, alisema "Naam, si desturi kwenu Wayahudi kuongea na mwanamke Msamaria hivi." Akasema, "Hatuchangamani moja kwa mwingine."

93 Akasema, "Lakini ungelijua ni Nani unayeongea naye, ungeliniomba Mimi maji, nami ningekuletea, ningekupa maji usije hapa kuteka."

94 Naam, yeye akasema, "Sasa ngoja kidogo." Akasema, "Sisi tunaabudia mle milimani, nanyi Wayahudi huabudia Yerusalemu."

95 Yesu akasema, "Lakini saa inakuja ambapo—ambapo hamtaabudia kule Yerusalemu wala katika mlima huu, bali

katika Roho; maana Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwambudu katika Roho na Kweli." Mnaona? Vema, Yeye aliendelea, na kuendeleza maongeo hata akatambua shida yake ilipokuwa. Nini, mwajua ilipokuwa shida ya huyo mwanamke kisimani? Yeye alikuwa na waume wengi zaidi, sivyo? Kwa hivyo Yeye akamwambia, "Nenda kamlete mume wako aje hapa."

Akasema, "Sina mume ye yote."

96 Kasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, naye uliye naye siye mume wako."

97 Akasema, "Bwana!" Sasa mtazame. "Bwana, naona ya kuwa u nabii." Ukifuatilia nyuma kule maandishi yaliyo kandoni mwa kurasa, utatambua, "Bwana," katika asili yake, "Wewe u... Naona kuwa Wewe u *yule* Nabii." Kumbukeni katika Biblia, ya kwamba alisema 'yule Nabii'? Je, Wewe ndiye 'yule Nabii'?" Alikuwa Nabii yupi? Ni yule ambaye Musa alisema angeinuliwa. "Naona ya kuwa Wewe u Nabii. Sasa, tumefundishwa, nasi tunajua Masihi ajapo Yeye atatenda mambo haya." Hiyo ndiyo ilikuwa ishara ya Masihi, sivyo, kujua shida zake zilikuwa nini? Kasema, "Tunajua Masihi ajapo Yeye atatwambia mambo haya. Lakini Wewe u nani?"

Yeye akasema, "Mimi ndiye ninenaye nawe."

98 Akaacha mtungi wake. Akakimbia mjini, nadhani, akiushikilia tu moyo wake, akisema...akishikilia mikono yake kifuani akirukaruka, akisema, "Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye yule Masihi? Je, si huyu ndiye yule Biblia ilisema angekuja? Ni Myahudi anayeketi pale, mtu wa kawaida, alionekana kama seremala. Lakini aliniambia kuwa nilikuwa na waume watano, nanyi nyote mwajua kuwa hii ni kweli. Huyu hana budi kuwa ndiye Masihi." Sivyo?

99 Sasa, Yesu alisema, "Kitambo kidogo, muda mchache, ulimwengu hautaniona tena. Bali ninyi mtaniona kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata ndani yenu. Na kazi nizifanyazo Mimi nanyi mtazifanya. Hata zaidi ya zile nimefanya hapa mtazifanya, maana nakwenda kwa Baba, nitarudi katika mfano wa Roho." Dhabihu imelipwa, yule Mzao wa Kifalme alikufa, yule mzao wa Kifalme alifufuka tena. Sasa Kanisa linasimama limehesabiwa haki kwa kuamini hilo, na yule Mzao wa Kifalme anaweza kuingia katika watu hawa hata kuwafanya warithi pamoja naye, wana wa kiume na wa kike wa Mungu.

100 Sasa, kwenu nje huko msio katika mstari wa maombi, nilimwambia yeye atoe tu kadi kwa watu ambao... Nilipompigia simu asubuhi ya leo, alikuwa amenipigia, kasema, "Unataka niende nikatoe kadi, baba?"

101 Nikasema, "Kukiweko watu wapatao kumi wanaotoka nje ya Maskani haya."

102 Sasa, wakati mwingine katika Maskani mimi huwaita na kuwapa kadi za maombi. Unarudi, ukisema, "Vema, yeye aliwajua, wao walikuwa wametoka kwenye Maskani. Alijua hali yao. Hakika."

103 Ndipo nageuka, nasema, "Wale tu wanaotoka nje ya Maskani, njooni. Vema, ninyi msio wa Maskani, mtakuwa ndinyi mtakaoingia katika mstari wa maombi."

104 "Lo, hatukuwajua," kasema Maskani. "Hatujui shida zao. Huenda yeye amekuwa akidanganya kuhusu hali zao, waona?"

105 Kisha nasema, "Asije mtu. Hebu Roho Mtakatifu awachague wale walio ndani humu wasio wa Maskani haya, wanaoketi mle tu." Bado ninyi mna . . .

106 Hamna njia yo yote ya kumleta mtu kwa Mungu isipokuwa Yeye amechaguliwa asili awe Mwana wa Mungu. Haiwezekani kamwe. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Na hiyo ni Kweli. Ch chote Yeye alichofanya, kulikuwa na jambo fulani kinyume. Kama angetenda *hivi*, ilipaswa kuwa *hivi*, na *hivi*, ilipaswa kuwa nyuma *vile*. Unaona, ni kutokuamini tu. Lakini hekima imehasibiwa haki na watoto wake. Kwa hivyo ninyi, mnaona.

107 Sasa hapa, ninajaribu ku—kuliambia kusanyiko hili la watu, haya, ya kwamba Yesu Kristo alikuwa ndiye yule Mzao wa Kifalme. Si sisi; ni Yeye. Sisi ni warithi tu wa hayo, lakini vitu vyote ni vyetu. Vipi kama Yeye angalisimama hapo siku hiyo Simoni alipokuja, nanyi, hamna mtu, hili ndilo jambo la kwanza alilopata kufanya?

108 Sasa, hilo litakuwa jambo la kwanza kwa watu hawa, kama Yeye akilifanya, wao hawajawahi kuliona hapo awali.

109 Lakini Simoni alipokuja, mvuvi mzee, hana elimu ya kutosha kuandika jina lake katika kijikaratasi. Biblia ilisema yeye alikuwa mtu asiye na elimu na asiye na maarifa, "na" ni kiunganishi, asiye na elimu na maarifa. Kisha Yeye alipotembea katika ishara ya . . .? . . . Yesu, Yesu alisema, "Jina lako ni Simoni." Wadhani aliwaza nini? Wewe ungaliwaza nini kama ungalikuwa umesimama hapo? "Na jina la baba yako ni Yona. Na tangu leo utaitwa Petro." Ungaliwaza nini? Je, Mtu huyu alikuwa akisoma mawazo yake? Vema, ungalidhania nini? Je, ungedhani kuwa hiyo ilikuwa ishara ya Masihi?

110 Ikiwa hiyo ndiyo ishara ya Masihi katika wakati mmoja, haina budi kuwa ishara ya Masihi ya wakati wa pili, wakati wa tatu, wakati wa nne, kila wakati lazima iwe vile vile, kwa sababu Mungu hawezi kubadilika. Na ni wangapi wanajua Masihi alikuwa Mungu? Hakika, alikuwa Mungu aliye na Upako. Hakika. Kwa hivyo Yeye hawezi kubadilika. Yeye hana budi kuwa yule yule.

111 Hiyo ndiyo sababu alipaswa kushuhudia jambo lile lile kwa Wasamaria ambalo alishuhudia kwa Wayahudi, kwa sababu yale mataifa matatu ya watu ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; Myahudi, Mtaifa, na Msamaria.

112 Sasa, mwatambua Roho Mtakatifu? Ni wangapi wanatambua Petro alikuwa na funguo za Ufalme? Je, mnatambua ya kwamba Yeye aliufungua katika siku ya Pentekoste, kwa Wayahudi? Filipo alishuka akaenda akawahubiria Wasamaria, akawabatiza katika Jina la Yesu Kristo; lakini Roho Mtakatifu hakuwa amewashukia bado; iliwabidi kutumana Petro aitwe, ambaye aliweka mikono yake juu yao, nao wakapokea Roho Mtakatifu. Hilo ni sawa? Na mle nyumbani mwa Kornelio, Ma—Mataifa wakampokea. Hivyo ndivyo ilivyokuwa, tangu hapo. Yesu alikuwa wazi kwa wote, naam basi. Unaona, Yeye alipaswa kuufungua. Mungu yuna njia za kutenda mambo.

113 Sasa, asubuhi ya leo, ikiwa Huyu aliyetoa ile ahadi kwa ule uzao na iwapo umeketi hapa (nataka kuamini kila mmoja wenu ni mmoja wao), iwapo ule uzao umeketi hapa, hakika huo uzao utaiona ile Ahadi. Sasa kila mmoja wa watu hawa wanaosimama hapa wameinua mikono yao, hawajawahi hata kuwa mkutanoni hapo mbeleni. Wao ni wageni kwangu. Simjui hata mmoja wao. Walikuja tu humu ndani, na dakika chache zilizopita Billy aliwapa kadi za maombi, ndio hawa wamesimama hapa. Kuna wengi wenu huko mlioinua mikono yenu, ambao hamkuwa na kadi ya maombi, nanyi mlikuwa mngali wageni hapa. Hayo si hoja. Amini tu kuwa wewe u mrithi wa ahadi hiyo. Amini tu kuwa kwa kupigwa Kwake uliponywa, na uamini hayo kwa moyo wako wote, kisha umtazame Yeye.

114 Jambo pekee kwa kipawa hiki, ni kujisalimisha tu Kwake. Sisemi neno, Yeye ndiye anayenena. Na ikiwa ni Roho Wake wa unabii, nabii kila mara alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Kila mara alikuwa sahihi. Na hakuna swali la Mafundisho kwa sababu ita—itapswa ilingane na Biblia, ikiwa ni Mungu. Mungu hawezi kusema jambo fulani halafu arudi tena akaligeuza. Yapasa liwe jambo lile lile wakati wote.

115 Sasa, ninyi nje huko, aminini kwa cho chote kilicho ndani yenu, ninyi aminini. Sasa msitembee po pote, ketini kwa utulivu sana sasa, kila mtu. Kwa upole na kimya mwezavyo. Inatokea kuwa, asubuhi hii, ya kwamba mtu wa kwanza anayesimama hapa ni mwanamume. Sasa tutachukua Andiko hili.

116 Sasa, mnaona ninaposimama? Ni wangapi wanaoweza kuelewa hilo? Hapa kuna wanaume na wanawake wanaosimama hapa ambao sijawaona maishani mwangu. Hata hawajapata kuwa mkutanoni, nanyi mwaona wanaposimama. Hawajui kitakachotendeka. Sijui kitakachotendeka. Lakini Mungu aliahidi! Ibrahimu hakujua kitakachotendeka alipochukua kisu

kile kumuua Isaka, lakini Mungu alimwahidi. Hilo lilitosha. Yeye alikuwa amempokea kama mtu aliyetoka kwa wafu, akijua Yeye aliweza kufufua toka kwa wafu. Sivyo? Kwa hivyo hilo latosha.

117 Sasa, hapa yuasimama mwanamume karibu nami, sijapata kumwona, sijui neno kumhusu. Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. Hatujuani. Mungu anatujua sote wawili. Sasa, kwa karama ya Kiungu, kama naweza kwa karama. . . Sasa, hizo karama unazaliwa nazo, Mungu alizikusudia asili kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Ni wangapi wanajua hilo? Kwa hivyo, si kitu cho chote nilichokuwa nacho ili nipate kuchukua karama hii, Mungu aliichagua. Sikuchagua hiyo; Yeye aliichagua. Mnaona? Kama manabii wa Agano la Kale, na watu mbalimbali, wao walikusudiwa asili kutenda hivyo, kutenda haya.

118 Sasa, kama mtu huyu ni mgonjwa, singeweza kumponya. Ikiwa mtu huyu ana haja itategemea kile anachohitaji kama ningeweza kumsaidia au la. Labda, kama ilikuwa jambo fulani kama yeye. . . jambo fulani dogo ningemsaidia, kwani, ningefurahi kumsaidia. Labda yeye ana hasira. Labda yeye hata si Mkristo. Labda ni Mkristo. Labda ni mlaghai. Sijui. Vipi kama yeye ni mnyemeleaji ashambulie, aliyekuja kisiri hapa, akijifanya mwenye kitu fulani; tazameni kile kitendekacho, mwaona, ki—kile tu kitukiacho. Mwaona? Sijui.

119 Lakini, tazama, wewe unasimama hapa, ndipo waweza kusimama ukijua kikamilifu, kwamba Mungu alitoa ahadi, Mungu hutimiza ahadi Yake. Waona? Sasa, ikiwa Mungu atatimiza ahadi Yake papa hapa sasa, kwa watu hawa, ni wangapi huko nje wataketi hapo nje, na kwa mioyo yao yote wataamini, kwa mioyo yenu yote mtaamini? Basi amininі tu.

120 Sasa, hebu tuone, na tuchukue Andiko moja. Sasa, Simoni Petro alimjia Bwana Yesu. Na alipofika tu kwa Bwana Yesu, Bwana Yesu akamwambia yeye alikuwa nani, na—na akamwambia mambo kuhusu maisha yake. Vema, Yesu yule yule yu aishi leo. Yeye, je, unaamini Yeye alifufuka katika wafu? Je, unaamini kuwa Roho huyo wa Kimasihi anaishi papa hapa Kanisani leo vivyo hivyo tu kama alivyokuwa daima? Vema.

121 Sasa, ninyi mlio makutanoni ambao hamna kadi za maombi, angalieni hapa na kusema, “Bwana!” Bila shaka, hamna kadi za maombi makutanoni, wote walio nazo wamesimama hapa. Wewe uliye makutanoni sema, “Bwana, niguse mimi.” Uone kitakachotendeka.

122 Sasa, bwana, kama kulikuwa na njia duniani ya kukusaidia, ningekusaidia. Waona, mimi niko tu, sisi tu wageni hapa, nami—nami ninakutana nawe kwa mara yangu ya kwanza. Lakini ni wajibu wangu, kama mhudumu, kunena Kweli na kuwa shahidi wa Yesu Kristo. Na, sasa, sitaki uniambie cho

chote. Nataka unijibu kama ni kweli ua la, ndipo umwache Yeye afanye hivyo. Na ikiwa Yeye atatenda sawasawa hapa jukwaani, kupitia kwa mwili huu, yale Yeye alitenda kupitia kwa mwili wa Yesu, huyo ni Mungu katika Kristo . . . Yesu alisema, "Sitendi lo lote mpaka Baba, ambaye yumo ndani Yangu, anionyeshe. Yeye huniambia la kutenda." Kwa hivyo haikuwa Yesu aliyemwambia mwanamke yule, ilikuwa ni Baba ndani Yake, aliyemwambia mwanamke huyo. Ilikuwa—haikuwa Yesu aliyejua Simoni alikuwa nani, ilikuwa ni Baba aliyeishi ndani Yake, aliyejua Simoni Petro alikuwa nani. Ndivyo hivyo, waona, ndivyo hivyo.

123 Naweza kukwambia sasa, wewe ni Mkristo, naam, bwana, kwa sababu una ro—roho ya ukarimu inayotetemeka kwa ukunjufu. Naye, yeye ni mwamini, yeye ni Mkristo. Na una wasiwasi unaokupa shida za tumbo. [Yule mgonjwa asema, "Ndivyo"—Mh.] Sivyo? ["Ndivyo"] Mnaona? Mnaona? Sasa, hilo ni sawa kabisa. Nili—nilijuaje hilo? Ningejuaje hilo ulimwenguni kote? Hatujaonana hapo mbeleni. Hilo ni kweli, sivyo? Labda Yeye atakwambia jambo lingine kukuhusu wewe. Nitakwambia, hapa kuna jambo fulani, namwona mwanamke karibu nawe. Yeye yuko pamoja nawe, ni mke wako. Yeye anahitaji msaada, pia. ["Hiyo ni kweli."] Naam, bwana. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida ya mke wako? ["Najua Yeye anaweza"] Vema, bwana. Yeye ana shida za moyo, matatizo. ["Naam, bwana."] Hiyo ni kweli, sivyo?["Ndivyo."] Wasiwasi pia. Naam, bwana. Sasa hutoki humu mjini; wewe hurudi *hivi* unapoenda nyumbani, ukienda Cincinnati. Hiyo ni kweli. Umetoka Cincinnati, Ohio. ["Naam, bwana."] Jina lako ni Milliken. Rudi, rudi nyumbani, ukapone. Bwana atakubariki nawe utapata afya, wewe pamoja na mkeo. Mungu akubariki.

Njoo, bwana. Unaamini? Sasa uwe tu na imani, usitie shaka.

124 Sasa mwe na kicho sana, kila mtu sasa, iweni tu na kicho sana, mwe kimya. Mnaona Roho Mtakatifu hushituka sana. Ni wangapi wanajua hilo? Anashituka kweli kweli, Roho Mtakatifu, waona, kukatizwa kudogo tu humsumbua Yeye.

125 Kulingana na madaktari, huna budi kufa mara moja, kwa shida za moyo. [Yule mgonjwa asema, "Naam"—Mh.] Ndivyo. Umekuja hapa kutoka Chicago Bw. Mosley. ["Naam"] Jina lako la kwanza ni Theodore. ["Naam."] Je, unaamini Mungu? ["Ndivyo"] Basi nenda nyumbani ukaishi katika Jina la Yesu Kiristo, ukopone. Mungu akubariki.

126 Je, unamwamini Mungu? [Yule mgonjwa asema, "Hakika namwamini. Naam, bwana"—Mh.] Unaumwa mguu. Wewe pia unatoka nje ya mji huu, ["Naam, bwana"] Unatoka Owensboro, Kentucky. Jina lako ni Bi. Lamb. ["Naam, bwana"] Rudi nyumbani ukapone.

127 Mwanamke anayeketi pale, pia anatoka Owensboro, ana jipu chini ya titi lako hapa, anatarajiwa kupasuliwa kesho. Enenda zako, amini, ukaishi.

128 Je, unaamini, Bwana? Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. Jina lako ni Bw. Gilroy. Hiyo ni kweli. Umetoka Anderson, Indiana, palipo lile dhehebu kuu la Church of God. Hiyo ni kweli. Umesimama hapa kwa ajili ya binti yako anayeteseka kwa sehemu. Yeye amepooza kwa sehemu. Waamini? Basi nenda zako nyumbani ukamkute jinsi unavyoamini. Vema, Mungu akubariki. Iweni na imani, amininі.

129 Je, unaamini kwa moyo wako wote, bwana? [Yule mgonjwa asema, "Naam, bwana"—Mh.] Unatoka Indianapolis. ["Naam"] Wewe ni mhudumu wa Injili. Huyo ni mke wako. A-ah. Yeye pia anaugua. Ana shida ya koo kooni. Daktari . . . Alikuwa na shida za moyo, ana wasiwasi kidogo. Naona yeye ni kiziwi katika . . . Njoo hapa. Asante. Ewe pepo wa uziwi, katika Jina la Yesu Kristo, nakuamuru kwa Mungu aliye hai, mtoke mwanamke huyu. Sasa wanisikia vizuri sasa. Nyote wawili mnaweza kwenda nyumbani mpate afya. Rudini nyumbani. mwenu. Mnasikia mmepona na mtapata afya.

130 Je, unaamini kwa moyo wako wote? Uwe tu na imani katika Mungu, amini.

131 Hiyo yabisi kavu ya kale na kadhalika ni kitu kibaya sana. Je, unaamini Mungu atakuponya? Basi pitia papo hapo uende nyumbani, lisifu Jina Lake, ukisema, "Asante, Mpendwa Bwana Yesu." Sababu ya kulipata hilo upesi sana, mwanamke huyu alikuwa na ugonjwa uo huo, yabisi kavu. Nawe unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, bwana, basi pitia papa hapa, na useme, "Asante, Ewe Bwana Yesu," kisha uende nyumbani.

132 Vema, dada geuka tu urudi, na uamini kuwa—kuwa ukavu ulio gotini mwako uko hapa, na ugonjwa wako wa moyo na kadhalika, geuka tu urudi nyumbani, useme, "Asante, Ewe Bwana Yesu," na upone. Amini kwa yote yaliyo ndani yako.

133 Unaamini? Na huko nje, je, wengine wenu mnaamini?

134 Msichana anayeketi pale, mwenye nywele nyeusi, una kifafa, je, unaamini kuwa Mungu atakuponya? Je, waukubali? Vema, ukiukubali, Yeye atafanya hivyo.

135 Hapa ameketi mhubiri anayeketi hapa. Anataka kutembea karibu na Mungu, sivyo, bwana? Je, unaamini Mungu atakutendea hayo? Inua mkono wako useme, "Naikubali." A—ah.

136 Maskini mwanamke huyu anayeketi hapa ameutelemsha mkono wake, ana matatizo ya kiroho anayowazia. Hiyo ni kweli.

137 Hapa kuna mwanamke hapa anashangaa iwapo atapata mtoto wake. Hiyo ni kweli. Umekuwa katika mojawapo wa

mikutano yangu. Nami nilikuahidi kwa Mungu, mtoto. Sivyo? Vema, basi nenda zako nyumbani ukampate. Usijisumbue juu yake tena.

138 Je, mnaamini kwa mioyo yenu yote, ninyi nyote? Kila mmoja wenu anaamini? Ule uzao wa Ibrahimu utamiliki mlango, mlango wa adui. Je, ninyi ni mzao wa Ibrahimu, kupitia kwa Yesu Kristo? Inueni mikono yenu ikiwa ndivyo mlivyo. Kisha weka mikono yako juu ya jirani yako, juu ya jirani yako, ninyi kwa ninyi. Wekeleaneni mikono. Milikini huo mlango sasa, ni wenu! Ni mali yenu. Kuomba kwa imani kutawaponya wagonjwa, Mungu atawainua. Vema, ombeni mnavyotaka. Ombeni jinsi muombavyo kanisani mwenu. Waombee watu walio pamoja nawe. Wekeleaneni mikono ninyi kwa ninyi na muombe.

139 Bwana Yesu, tunakuja katika Jina hilo kuu lenye Nguvu sana la yule Mzao wa Kifalme, yule Mzao wa Ibrahimu, aliyeahidiwa kule mlimani ulipomtoa yule mwana-kondoo; na ukamweka huyo mwana-kondoo jangwani, jambo la kisiri, sawa na ulivyofanya kwa wale kindi jana. Naomba, Ee, Bwana Mungu, ya kwamba utaituma nguvu, imani, na ukubalie kila mzao... Najua watafanya hivyo, Bwana, kwa maana Wewe ulisema, "Ule uzao wa Ibrahimu!" Na kama kumekuwa na baadhi yao hapa ambao wamekuwa wakijifanya kuwa ule uzao, na si uzao huo, wasamehe kwa kukusudia kwao hapa ama kujifanya, na Roho Mtakatifu sasa akawashe moto nafsi zao kwa imani iliyo hai. Hebu Roho Mtakatifu na apenyeze katika kila moyo na amponye kila mtu hapa. Wamewekeleana mikono yao mmoja juu ya mwingine. Yule Mzao wa Kifalme alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Na Yeye Yule aliyeahidi yu hapa sasa hivi, akijionyesha Mwenyewe kuwa yuko hapa. Uzao uko hapa huku wamewekeleana mikono yao wao kwa wao. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Roho Mtakatifu na apitie kila mmoja wa mikono yao, hadi mioyoni mwa watu, hadi miilini mwao, na aponye kila mmoja aliye katika Uwepo wa Kiungu. Tujalie, Bwana. Namkemea Shetani, nakemea kutokuamini kwote, nakemea kila pepo mchafu, namkemea kila mwenye kujifanya, nakemea kila kitu kilicho kinyume cha Neno la Mungu. Na Roho Mtakatifu apachukue mahali Pake mioyoni mwa watu sasa hivi, kwa imani. Na kila ugonjwa na kila maradhi, kila teso, na yawaondokee watu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

140 Sasa, uzao wa Ibrahimu, ninyi ni ukoo wa kifalme, ninyi ndio ile ahadi. Kwa neema na kwa msaada wa Mungu, ni wangapi waweza kuinua mikono yao na kusema, "Nimepokea kile nilichoomba." Asanteni. Ndivyo hivyo. Hiyo ndiyo sababu ya ahadi. Hiyo ndiyo sababu ya kutolewa kwa ahadi, upate kuwa mrithi wa mambo yote, katika Yesu Kristo aliyekuokoa. Yeye

alikuokoa toka dhambini, alikuokoa na magonjwa, alikuokoa na mauti, alikuokoa na jehanamu, alikuokoa na kaburi.

141 Mnasema, "Ndugu Branham, lakini sisi sote huenda kaburini." Lakini kaburi haliwezi kutushikilia. Yeye alienda mle pia, bali halingeweza kumshikilia. Bila shaka haliwezi kumshikilia.

142 "Vema, Ndugu Branham, nimejaribiwa sana." Yeye alijaribiwa pia. Lakini alikuokoa wewe na majaribu.

143 "Usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu." Unaona, Yeye alitenda hayo! Yote ni yako. Kila kitu ni chako, kwake Yesu Kristo. Yeye hukupa kila kitu bure. Hamna malipo kwake, hata kidogo. Ni vyako hivi sasa. Je, huna furaha kwa ajili yake? Je, haumfurahii Yeye? Mungu apewe shukurani.

144 Sasa, kutakuwa na ibada usiku wa leo, ni—ni usiku wa leo, saa moja na nusu za usiku. Nitaacha mchungaji awaambieni. Njoo, njoo. Basi, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda nitarudi kuwaombea wagonjwa hapa Maskanini, au po pote pale.

*Kumiliki Malango Ya Adui* SWA59-1108
(Possessing The Enemy's Gates)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Novemba 8, 1959, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org